# MAJADILIANO YA BUNGE

(HANSARD)

TAARIFA RASMI

---

BUNGE LA NNE

(MKUTANO WA KWANZA)

TAREHE

6 Nov.—8 Nov., 1975

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| | SAFU |
| Orodha ya Wajumbe wa Bunge ... | v |
| **ALHAMISI, TAREHE 6 NOVEMBA, 1975** | |
| Uchaguzi wa Spika ... | 1 |
| Matokeo ya Uchaguzi wa Spika ... | 1 |
| Kiapo cha uaminifu ... | 2 |
| Kuongeza muda wa kukaa Bunge ... | 4 |
| Uchaguzi wa Naibu wa Spika ... | 5 |
| Matokeo ya Uchaguzi wa Naibu wa Spika ... | 5 |
| Kuahirisha Bunge ... | 12 |
| **IJUMAA, TAREHE 7 NOVEMBA, 1975** | |
| Kiapo cha Uaminifu ... | 13 |
| Uchaguzi wa Wabunge wa Taifa wa Mikoa ... | 13 |
| Uchaguzi wa Wabunge wa Taifa waliopendekezwa na Mashirika ... | 13 |
| Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria la Afrika Mashariki ... | 13 |
| **MATOKEO YA UCHAGUZI WA WABUNGE** | |
| Wajumbe wa Taifa wa Mikoa ... | 16 |
| Wajumbe wa Taifa wa Mashirika ... | 17 |
| Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria la Afrika Mashariki ... | 17 |
| Kuahirisha Bunge ... | 17 |
| **JUMAMOSI, TAREHE 8 NOVEMBA, 1975** | |
| Kiapo cha Uaminifu ... | 19 |
| Kuahirisha Bunge ... | 19 |

## ORODHA YA WAJUMBE WA BUNGE LA TANZANIA

**Spika**

Ndugu Mtwa Adam Sapi Mkwawa

**Wajumbe**

| | (Jimbo la Uchaguzi) |
|---|---|
| Ndugu Aboud Jumbe | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Rashid Mfaume Kawawa | *Liwale* |
| Ndugu Mohamed Abdulla | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Rashid Abdulla | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Ali Abeid | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Aboud Talib Aboud | *Kateuliwa Zanzibar* |
| Ndugu John Michael Aidi | *Mbunge wa Taifa/Lindi* |
| Ndugu Ibrahim Saadala Akida | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Ali Mzee Ali | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Bakari Jabu Ali | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Khamis Ali | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Muhsin Bin Ali | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Tabu M. Alli | *Kateuliwa* |
| Ndugu Hamid Ameir | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Seleiman Ameir | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Stephene Phillip Assey | *Mbunge wa Taifa/Dodoma* |
| Ndugu Edward Barugini Muyagi Barongo | *Mbunge wa Taifa/Ziwa Magharibi* |
| Ndugu Michael Gabriel Lijeje Lyanga Baruti | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Said Idi Bavuai | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Mwinyimvua Bohari | *Morogoro Vijijini* |
| Ndugu Mtumwa Boraafya | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Dereck Noel Maclean Bryceson | *Kinondoni* |
| Ndugu Ali Saidi Bungara | *Kilwa* |
| Ndugu Corona Faide Busongo | *Mbunge wa Taifa/Mwanza* |
| Ndugu Adam Chobaliko Bwenda | *Kasulu* |
| Ndugu Wilbert Chagula | *Kateuliwa* |
| Ndugu Mboni O. Cheka | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Jacob John George Chibwana | *Tunduru* |
| Ndugu Margaret Chogo | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Henry O. Clemens | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Ahmed Amri Dodo | *Hanang* |
| Ndugu Isael Nyaka Elinawinga | *Hai* |
| Ndugu Frederick Ntemiriyanda Fumbuka | *Shinyanga Mjini* |
| Ndugu Mujengi Mange Gwao | *Singida Vijijini* |
| Ndugu Mkubwa Haji | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Mary Edith Hancock | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Mubula S. Hassani | *Geita* |
| Ndugu Amiri Kingazi Hoza | *Lushoto* |
| Ndugu Ismail Salehe Ismail | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Itala Francis Itala | *Mbunge wa Taifa/Rukwa* |
| Ndugu Amir Habib Jamal | *Morogoro Mjini* |

| | (Jimbo la Uchaguzi) |
|---|---|
| **Ndugu** Ana Kabati | *Kateuliwa* |
| **Ndugu** Leonard Manwa Kaboboye | *Mbunge wa Taifa/Kigoma* |
| **Ndugu** Ibrahim Mohamed Kaduma | *Mbunge wa Taifa/Iringa* |
| **Ndugu** Ibrahim Sufian Alli Kajembo | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Philbert Bashiganye Kapunda | *Magu* |
| Ndugu Kapteni Musa Ramadhani Kassanda | *Tabora Vijijini* |
| Ndugu Stanislaus Rugaba Kasusura | *Biharamulo* |
| Ndugu Ali Hassan Khamis | *Kateuliwa Zanzibar* |
| Ndugu Mkuja Suleiman Khamis | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Tawakali Khamis | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Rashidi Nassoro Kibendera | *Kisarawe* |
| Ndugu Emmanuel Kibira | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Johnson Wallace Kihampa | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Charles Kileo | *Katibu wa Mkoa* |
| Meja Muhidin Kimario | *Moshi Mjini* |
| Meja Ayub Shomari Kimbau | *Mafia* |
| Ndugu Abdallah Mohamed Kimosa | *Kiteto* |
| Ndugu Dk. Kingwaba Hassan Kingwaba | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Mwanjes Leopold Kintu | *Bukoba Vijijini* |
| Ndugu Herman Kyanzi Daniel Kirigini | *Musoma Vijijini* |
| Ndugu Mohamed Nassor Kissoky | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Peter Kisumo | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Joseph Gabriel Kitigwa | *Tarime* |
| Ndugu Kasmiri Yohani Komba | *Mbunge wa Taifa/Pwani* |
| **Ndugu** Alli Kombo | *Katibu wa Mkoa* |
| **Ndugu** Sheikh Thabit Kombo | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Kitwana Selemani Kondo | *Ilala* |
| **Ndugu** Nicholas Kuhanga | *Mbunge wa Taifa* |
| **Ndugu** Mahami Rajabu Kundya | *Singida Mjini* |
| **Ndugu** Hindu Lila | *Mbunge wa Taifa* |
| **Ndugu** Ntambala Samuel Luangisa | *Bukoba Mjini* |
| Ndugu Rashidi Lukandamila | *Kigoma Vijijini* |
| **Ndugu** Yahaya Bakari Lukoya | *Mbunge wa Taifa/Tanga* |
| **Ndugu** Vennant Joseph Lwabuti | *Karagwe* |
| **Ndugu** Anselm Ngonyani Lyander | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Joseph Eugene Macha | *Moshi Vijijini* |
| Ndugu Peter Macha | *Mbunge wa Taifa/Dar es Salaam* |
| Ndugu Ayoub Machano | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Khamis Machano | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Daniel Madaha Machemba | *Mwanza* |
| Ndugu Joseph Sereri Magoto | *Serengeti* |
| Ndugu Daud Mahmoud | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Mohamed Mahmoud | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Edgar Diones Maokola Majogo | *Nachingwea* |
| Ndugu Hasnu Makame | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Juma Makame | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Anna Makinda | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Ibrahim Makungu | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Jackson Makweta | *Njombe* |

| | (Jimbo la Uchaguzi) |
|---|---|
| Ndugu John William Samwel Malecela | *Dodoma Vijijini* |
| Ndugu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya | *Muheza* |
| Ndugu Julie Manning | *Kateuliwa* |
| Ndugu Gisler Mapunda | *Songea Mjini* |
| Ndugu Edward Ng'hwami Masanja | *Bariadi* |
| Ndugu Kassim Ali Masego | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Mussa Sefu Massomo | *Handeni* |
| Ndugu Richard Mazengo | *Mpwapwa* |
| Ndugu Osiah Exson Abnezer Mbembela | *Ileje* |
| Ndugu Jacob Maswa Sumbi Mbutu | *Katibu wa Mkoa* |
| Meja Ali Saidi Mchumo | *Temeke* |
| Ndugu Mohamed Mfaume | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Yohana Chediel Mgonja | *Pare na Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Geoffrey Oscar Mhagama | *Songea Vijijini* |
| Ndugu John Edward Fumbwe Mhina | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Padri Paulo Isai Misigalo | *Tabora Mjini* |
| Ndugu Hemed Bakari Mkali | *Rufiji* |
| Ndugu Hassan Nassor Hassan Moyo | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Adrian Adreas Mpande | *Bagamoyo* |
| Ndugu Titus Mpanduji | *Kateuliwa* |
| Ndugu Afra Gabriel Mpiri | *Lindi Vijijini* |
| Ndugu A. R. Msangi | *Mbunge wa Taifa/Kilimanjaro* |
| Ndugu Cleopa Msuya | *Kateuliwa* |
| Ndugu Damian Daftali Mtwanga | *Ifakara* |
| Ndugu Godfrey Protas Mugissa | *Ukerewe* |
| Ndugu Alhaj Omari Ahmed Muhaji | *Tanga* |
| Ndugu Mamdan Muhiddin | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Ali Mushin | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Joseph James Mungai | *Mufindi* |
| Ndugu John Benedict Mwakangale | *Rungwe* |
| Ndugu Richard Tupilike Mwakasege | *Mbeya Mjini* |
| Ndugu Daudi Ngelautwa Mwakawago | *Iringa Mjini* |
| Ndugu Jackson Wilfred Mwakibwili | *Mbunge wa Taifa/Mbeya* |
| Ndugu Wilfred Ephreim Mwakipesile | *Kyela* |
| Ndugu Felix Tadeo Mwanambilimbi | *Chunya* |
| Ndugu Abel Kyagunya Mwanga | *Musoma Mjini* |
| Ndugu Tobi Tajiri Mweri | *Pangani* |
| Ndugu Ali Hassan Mwinyi | *Kateuliewa—Zanzibar* |
| Ndugu Ali Mwinyigogo | *B.L.M.—Zanzinar* |
| Ndugu Chrisant Majiyatanga Mzindakaya | *Sumbawanga Vijijini* |
| Ndugu Daud Makenga Mzukila | *Nzega* |
| Ndugu Alhaj Maalim Sinani Nabahan | *Lindi Mjini* |
| Ndugu Yusufu Hamisi Nabalang'anya | *Mtwara Vijijini* |
| Ndugu Albert Larwence Nachunga | *Masasi* |
| Ndugu Anna Asher Namilikwa | *Mbunge wa Taifa/Singida* |
| Ndugu Stephen Salimu Nandonde | *Newala* |
| Ndugu Masanja Francis Nchimani | *Kwimba* |
| Ndugu Margaret John Ndaga | *Manyoni* |
| Ndugu Phillipo Ndaki | *Mbunge wa Taifa* |

| | (Jimbo la Uchaguzi) |
|---|---|
| Ndugu Paul James Casmir Ndobho | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Leonsi Ngalai | *Rombo* |
| Ndugu Kingunge Ngombale-Mwiru | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Robert Ng'itu | *Mbunge wa Taifa/Mtwara* |
| Ndugu Venance Ngula | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Said Ngw'anangw'alu | *Mbunge wa Taifa/Shinyanga* |
| Ndugu Nasania Robert Nkurlu | *Iramba* |
| Ndugu Kabenga Nsa-Kaisi | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Patrick Adam Nswila | *Mbeya Vijijini* |
| Ndugu Mustafa Salum Nyang'anyi | *Kondoa* |
| Ndugu Joseph K. Nyerere | *Mbunge wa Taifa/Mara* |
| Ndugu Nazar Gervas Nyoni | *Mahenge* |
| Ndugu Edward Elikana Bukumba Nzingula | *Shinyanga Vijijini* |
| Ndugu Solomon Alexander Ole-Saibull | *Arusha* |
| Ndugu Mwahija Rashidi Parangwa | *Kibaha* |
| Ndugu John Sibumbu Pembe | *Mpanda* |
| Ndugu Said Pongwa | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Patrick Sylverius Qorro | *Mbulu* |
| Ndugu Mosi Ramadhani | *Mbunge wa Taifa/Tabora* |
| Ndugu Ahmad Suleiman Riyamy | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Alphonce Marianus Rulegura | *Sengerema* |
| Ndugu Joseph Clemens Rwegasira | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Khamis Saburi | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Jeremiah Ngilambe Justine Saileni | *Kilosa* |
| Meja Jenerali Mirisho Sam Hagai Sarakikya | *Meru* |
| Ndugu Andrew Louis Sazia | *Kahama* |
| Ndugu Gwassa Angus Sebabili | *Ngara* |
| Ndugu Zaituni F. Selemani | *Mbunge wa Taifa/Ruvuma* |
| Ndugu Issac Abraham Sepetu | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Shah Kombo Shah | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Ali Sharif | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Issa Sharriff | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Hossein Ramadhani Shekilango | *Korogwe* |
| Ndugu Ali Abdallah Shaibu | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Simenti Costantine Shillingi | *Maswa* |
| Ndugu Lawi Nangwanda Sijaona | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Petro Yohana Simalenga | *Ludewa* |
| Ndugu Col. Tumbukiza Ayubu Mwinyimvua Simba | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Donatius John Simya | *Sumbawanga Mjini* |
| Ndugu Samuel John Sitta | *Urambo* |
| Ndugu Tabitha Siwale | *Kateuliwa* |
| Ndugu Peter Saidi Siyovelwa | *Iringa Vijijini* |
| Ndugu Blazio Katura Sizimwe | *Kibondo* |
| Ndugu Edward Moringe Sokoine | *Monduli* |
| Ndugu Mustafa Mohammed Songambele | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Rev. Severino Supa | *Dodoma Mjini* |
| Ndugu Dk. Leader Stirling | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Abdulnuru Suleiman | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Hadija Swedi | *Kateuliwa* |

| | |
|---|---|
| | (Jimbo la Uchaguzi) |
| Ndugu Alfred Cyril Tandau ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mbinga* |
| Ndugu Dk. A. J. Temu ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Crispin Tungaraza ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Alson Yilando Twinzi ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mbozi* |
| Ndugu Mwinchum Vuai ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Kateuliwa—Zanzibar* |
| Ndugu Richard Wambura ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Ezekiel Waryuba ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mbunge wa Taifa* |
| Ndugu Said Washoto ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *B.L.M.—Zanzibar* |
| Ndugu Stephen Masato Wassira ... ... ... ... ... ... ... ... | *Katibu wa Mkoa* |
| Ndugu Losa Yemba ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Kigoma Mjini* |
| Ndugu Khalid Mohamed Zalari ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mtwara Mjini* |
| Ndugu David Bakanyoma Simeo Zimbihile ... ... ... ... ... ... ... ... | *Muleba* |
| Ndugu Humbi Ziota ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Igunga* |
| [Wazi] ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Mbunge wa Taifa/Arusha* |

---

| | |
|---|---|
| Ndugu W. J. Maina ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... | *Katibu wa Bunge* |

## BUNGE LA NNE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

**Kikao cha Kwanza—Tarehe 6 Novemba, 1975**

(*Mkutano ulianza saa tatu asubuhi*)

### DUA

*Katibu wa Bunge (Nd. W. J. Maina) alisoma Dua.*

### UCHAGUZI WA SPIKA

**Katibu wa Bunge:** Nd. Wabunge sasa mtagawiwa karatasi za kura kwa ajili ya uchaguzi wa Spika. Tunaomba kila mmoja aandike jina moja la mtu ambaye anamwona anastahili kuwa Spika wa Bunge hili.

(*Hapa karatasi za kupigia kura ziligawiwa kwa Wabunge*)

**Katibu wa Bunge:** Nd. Wabunge sasa tumekwishapata kura zote hapa na tunaomba Nd. Rashid Abdulla na Nd. Kitwana Selemani Kondo watusaidie katika kuhesabu hizi kura.

(*Hapa kura zilianza kuhesabiwa*)

### MATOKEO YA UCHAGUZI

**Katibu wa Bunge:** Nd. Wabunge baada ya kuhesabu kura, yafuatayo ndiyo matokeo:

Chief Adam Sapi Mkwawa amepata kura 163. (*Makofi.*)

Chief Erasto Andrew Mbwana Mang'enya amepata kura 1. (*Makofi.*)

Hakuna kura hata moja iliyoharibika. (*Makofi.*) Kwa hivyo, Chief Adam Sapi Mkwawa ndiye amechaguliwa kuwa Spika wetu. Kwa hivyo naomba Wabunge wawili wakamtafute huko aliko ili aje kuapishwa. Nawaomba Sheikh Thabit Kombo na Chief Erasto Andrew Mbwana Mang'enya wakamtafute. (*Kicheko na Makofi.*)

*Hapa Spika (Nd. Adam Sapi Mkwawa)* ***aliingia*** *Bungeni akisindikizwa na Nd. Sheikh Thabit* ***Kombo*** *na Nd. E. A. M. Mang'enya, na baada ya* ***kuapa*** *alikalia kiti chake.*

### KIAPO CHA UAMINIFU

Wabunge wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi zao katika Bunge.

Nd. Aboud Jumbe.

Nd. Rashid Mfaume Kawawa.

**Spika:** Ndugu Wabunge tunayo orodha ya kuwaapisha Ndugu Wabunge na sasa atafuata Sheikh Thabit Kombo halafu tutaendelea na orodha kama inavyoonyesha.

Nd. Sheikh Thabit Kombo Jecha.

**Spika:** Ndugu Wabunge. katika orodha yenu hakuna masahihisho. Kwa kufuata orodha yangu atafuata Nd. Abdulnuru Suleiman halafu tutaendelea na orodha inavyotueleza.

Nd. Abdulnuru Suleiman.
Nd. Mohamed Abdulla.
Nd. Rashid Abdalla Ismail.
Nd. Ali Abeid Nasir.
Nd. Aboud Talib Aboud.
Nd. Ali Mzee Ali.
Nd. Bakari Jabu Ali.
Nd. Khamis Ali.
Nd. Muhsin Bin Ali.
Nd. Hamid Ameir Ali.
Nd. Suleiman Ameir Suleiman.
Nd. Michael Gabriel Lijeje Lyangu Baruti.
Nd. Said Idi Bavuai.
Nd. Mwinyimvua Bohari.
Nd. Mtumwa Boraafya.
Nd. Dereck Noel Maclean Bryceson.
Nd. Saidi Ali Bungara.
Nd. Adam Chobaliko Bwenda.
Nd. Wilbert Kumalija Chagula.

**Spika:** Ndugu Wabunge nitaliahirisha Bunge kwa muda mfupi ili nipate nafasi ya kumsindikiza Ndugu Makamu wa Kwanza wa Rais.

(*Saa tatu na dakika hamsini na tano Bunge lilifungwa kwa muda mfupi*).

(*Saa nne na dakika kumi Bunge lilirudia*)

Nd. Jacob John George Chibwana.
Nd. Ahmed Amri Dodo.
Nd. Isael Nyaka Elinawinga.
Nd. Frederick Nteminyanda Fumbuka.
Nd. Mujengi Mange Gwao.
Nd. Mkubwa Haji.
Nd. Amiri Kingazi Hoza.
Nd. Amiri Habib Jamal.
Nd. Ana Kabadi.
Nd. Ibrahim Sufian Ali Kajembo.
Nd. Philbert Bashinganye Kapunda.
Nd. Kapteni Musa Ramadhani Kassanda.
Nd. Stanislaus Rugaba Kasusura.

[Spika]
Nd. Ali Hassan Khamis.
Nd. Mkuja Suleiman Khamisi.
Nd. Tawakali Khamis.
Nd. Rashidi Nassoro Kibendera.
Nd. Johnson Wallace Kihampa.
Nd. Charles Kileo.
Nd. Meja Muhidin Mfaume Kimario.
Nd. Meja Ayub Shomari Kimbau.
Nd. Abdallah Mohamed Kimosa.
Nd. Kingwaba Hassan Kingwaba.
Nd. Mwanjes Leopold Kintu.
Nd. Herman Kyanzi Daniel Kirigini.
Nd. Mohamed Nassor Kissoky.
Nd. Peter Abdallah Kisumo.
Nd. Joseph Gabriel Kitigwa.
Nd. Ali Kombo.
Nd. Shah Kombo Shah.
Nd. Kitwana Selemani Kondo.
Nd. Mahami Rajabu Kundya.
Nd. Ntambala Samuel Luangisa.
Nd. Rashidi Mohamed Lukandamila.
Nd. Venant Joseph Lwabuti.
Nd. Mubula Salum Hassani
Nd. Joseph Eugene Macha.
Nd. Ayoud Machano Kiasi.
Nd. Khamis Machano Yusuf.
Nd. Daniel Madaha Machemba.
Nd. Joseph Sereri Magoto.
Nd. Daud Mahmoud Jecha.
Nd. Mohamed Mahmoud.
Nd. Edgar Diones Maokola Majogo.
Nd. Hasnu Makame Mwita.
Nd. Juma Makame Abdallah.
Nd. Ibrahim Kibwana Makungu.
Nd. Jackson Luvangila Makweta.
Nd. John Malecela.
Nd. Tabu Mamampakani Ali.
Nd. Erasto Andrew Mbwana Mang'enya.
Nd. Julie Catherine Manning.
Nd. Gisler Mapunda.
Nd. Ewdard Masanja Ng'havami.
Nd. Kassim Ali Masege.
Nd. Mussa Seffu Massomo.
Nd. Richard Mazengo.
Nd. Osiah Exson Abnezer Mbembela.
Nd. Jacob Sumbi Maswa Mbutu.
Nd. Ali Saidi Mchumo.
Nd. Mohamed Mfaume.
Nd. Chediel Yohana Mgonja.
Nd. Geoffrey Oscar Mhagama.
Nd. John Edward Fumbwe Mhina.
Nd. Padri Paulo Isai Misigalo.
Nd. Hemed Bakari Mkali.
Nd. Hassan Nassor Hassan Moyo.
Nd. Adrian Andreas Mpande.
Nd. Afra Gabriel Mpiri.
Nd. Cleopa David Msuya.
Nd. Damian Daftali Mtwanga.
Nd. Godfrey Protas Mugissa.
Nd. Omari Ahmed Muhaji.
Nd. Hamdan Muhiddin.
Nd. Ali Muhsin Bin Ali.
Nd. Joseph James Mungai.
Nd. John Benedict Ugogo Mwakangale.
Nd. Richard Tupilike Kipengele Mwakasege.
Nd. Daudi Ngelautwa Mwakawago.
Nd. Wilfred Ephreim Mwakipesile.
Nd. Felix Tadeo Mwanambilimbi.
Nd. Abel Kyagunya Mwanga.
Nd. Tobi Tajiri Mweri.
Nd. Ali Hassan Mwinyi.
Nd. Ali Mwinyikondo Mwinyigogo.
Nd. Chirsant Majiyatanga Mzindakaya.
Nd. Daud Makenga Mzukila.
Nd. Maalim Sinani Nabahan.
Nd. Yusufu Hamisi Yusufu Nabalang'anya.
Nd. Albert Lawrence Nachunga.
Nd. Stephen Salimu Nandonde.
Nd. Francis Nchimani Masanja.
Nd. Margaret John Ndaga.
Nd. Paul James Casmir Ndobho.
Nd. Leonsi Ngalai.
Nd. Kingunge Ngombale-Mwiru.
Nd. Nasania Robert Nkurlu.
Nd. Nsa-Kaisi Kabenga.
Nd. Patrick Adam Nswila.

## HOJA YA KUENDELEZA MUDA WA KUKAA

**Spika:** Ndugu Wabunge, Ninamwomba Makamu wa Rais wa Chama cha TANU atoe hoja ili tuendelee na shughuli yetu.

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, kwa sababu bado kazi yetu ya kuapa haijamalizika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge liendelee kukaa mpaka shughuli hizi za kuapa zimemalizika. (*Makofi.*)

Vile vile ninataka kutoa taarifa juu ya shughuli yetu ile ya jioni na sasa nashauri kwamba iwe saa kumi jioni. (*Makofi.*) Na Bunge likutane saa mbili usiku kwa ajili ya kupiga kura.

**Katibu wa Mkoa wa Kilimanjaro:** Nd. Spika, ninaafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

Nd. Mustafa Salum Nyang'anyi.
Nd. Nazar Gervas Nyoni.
Nd. Edward Elikana Bugumba Nzingula.
Nd. Solomon Alexander Ole-Saibul.
Nd. Mwahija Rashidi Parangwa.
Nd. John Sibumbu Pembe.
Nd. Said Pongwa Said.
Nd. Patrick Sylverius Qorro.
Nd. Ahmad Suleiman Riyamy.
Nd. Alphonce Marianus Rulegura.
Nd. Joseph Clemens Rwegasira.
Nd. Ibrahim Saadalla Akida.
Nd. Khamis Saburi Khamis.
Nd. Jeremiah Ngilambo Justino Saileni.
Nd. Meja Jenerali Mirisho Sam Hagai Sarakikya.
Nd. Louis Andrew Sazia.
Nd. Gwassa Angus Sebabili.
Nd. Issac Abraham Sepetu.
Nd. Sheikh Alli Shariff Mussa.
Nd. Alhaj Issa Sharrif Musa.
Nd. Hossein Ramadhani Shekilango.
Nd. Ali Abdallah Shibu.
Nd. Simenti Constantine Shillingi.
Nd. Lawi Nangwanda Sijaona.
Nd. Petro Yohana Simalenga.
Nd. Col. Tumbukiza Ayubu Mwinyimvua Simba.

Nd. Donatius John Simya.
Nd. Samuel John Sitta.
Nd. Tabitha Siwale.
Nd. Peter Saidi Siyovelwa.
Nd. Blazio Katura Sizimwe.
Nd. Edward Moringe Sokoine.
Nd. Mustafa Mohammed Songambele.
Nd. Padri Severino Supa.
Nd. Hadija Swedi.
Nd. Alfred Cyril Tandau.
Nd. Alson Yilande Twinzi.
Nd. Mwinchum Vuai.
Nd. Richard Saimora Wambura.
Nd. Said Washoto.
Nd. Stephen Masato Wassira.
Nd. Losa Kyomba Yemba.
Nd. Khalid Mohamed Zalari.
Nd. David Bakanyoma Simeo Zimbihile.
Nd. Humbi Ziota.

**Nd. Spika:** Ndugu Wabunge baada ya kiapo nafikiri ni nafasi nzuri kwangu niseme machache kuwashukuru. Kwa kifupi nasema hivi: chini ya uongozi wa Chama chetu kitukufu cha TANU na Afro-Shirazi nawashukuru kwa dhati kwa kunichagua mara nyingine tena kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi.*) Nitajitahidi kushirikiana na ninyi Ndugu Wabunge kudumisha heshima na hadhi ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi.*) Sina mengi ya hayo. (*Makofi.*)

## UCHAGUZI WA NAIBU WA SPIKA

**Katibu wa Bunge:** Ndugu Wabunge utaratibu ni kwamba mtagawiwa karatasi za kura na kila Mbunge ataandika jina la Mbunge mmoja anayemfikiria kuwa Naibu wa Spika.

(*Hapa karatasi za kura ziligawiwa na Wabunge walipiga kura zao*)

**Nd. Spika:** Namchagua Nd. Ahmad Suleiman Riyamy na Nd. Mwanjes Leopold Kintu ili wakasaidiane na Katibu wa Bunge kuhesabu hizo kura.

## MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU WA SPIKA

**Nd. Spika:** Ndugu Wabunge, matokeo ya kuhesabu kura, katika uchaguzi wa Naibu wa Spika, ni kwamba hakuna kura zilizoharibika, na Nd. Humbi Ziota amepata kura mbili, na Chifu Stanislaus Kasusura amepata kura 147. (*Makofi.*) Kwa hiyo Nd. Stanislaus Kasusura kachaguliwa kuwa Naibu wa Spika.

Ningependa kuchukua nafasi hii kutangaza kwamba nimewateua Nd. Humbi Ziota na Nd. Nabahan kuwa Wasaidizi wa Spika. (*Makofi.*)

Sasa namwomba Nd. R. M. Kawawa, ikiwa kama Makamu wa Rais wa Chama cha TANU, atukaribishe sisi Wabunge katika Bunge hili jipya. (*Makofi.*)

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, nao mba kuchukua nafasi hii baada ya kuchaguliwa wewe na baada ya sisi wote kuapa na baada ya kumchagua Naibu wa Spika, kwa niaba ya Nd. Wabunge wote na kwa niaba ya Taifa zima, nikupongeze kuchaguliwa kwako kuwa Spika wetu. (*Makofi.*) Nafanya hivyo, Nd. Spika, kama Makamu wa Chama. Nd. Spika, Tanzania tunaelewa uwezo tulionao wa kulitumikia Taifa letu. Kwa muda mrefu umekuwa kiongozi wa Bunge hili isipokuwa kwa kipindi cha muda mfupi ulipoteuliwa na Baba wa Taifa kuwa Waziri wa Ustawishaji Makao yetu Makuu mapya. Kazi ambayo umeifanya kwa juhudi na moyo mkubwa. (*Makofi.*) Katika muda wako wa kuwa Waziri hukupumzika kazi ya Bunge kwani tulikuwa nawe hapa. Lakini tunatumaini umepumzika vya kutosha kukalia kiti hiki. (*Kicheko.*) Na sasa utaanza na nguvu mpya. Tunakutakia heri katika kazi hii ya kuliongoza Bunge letu.

Naomba vile vile, Nd. Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Chifu Mange'nya kwa kazi yake njema ya kuliongoza Bunge hili. (*Makofi.*) Chifu Mang'enya alikuwa Naibu wako ulipokuwa Spika hapo awali. Bila shaka ulipokuwa hupo pamoja nasi, uliangalia vizuri shughuli zake za kazi ya Spika; na natumaini utakubaliana nami kuwa Chifu Mang'enya alitimiza wajibu wake vizuri. (*Makofi.*) Mimi nikiwa kama kiongozi wa shughuli za Serikali katika Bunge lililopita nakumbuka vizuri sana ushirikiano mzuri nilioupata kutoka kwake hata shughuli za Serikali zikaweza kujadiliwa kwa kikamilifu ndani ya Bunge hili. (*Makofi.*) Ahsante sana Chifu Mang'enya. Pole kwa msukosuko wa uchaguzi. (*Kicheko.*) Nakuombea heri katika kazi yako ya kushirikiana tena na Watanzania wenzako katika kulijenga taifa letu. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Nd. Kasusura kwa kuchaguliwa tena kuwa Naibu wa Spika. (*Makofi.*) Yeye tunamfahamu kwa uhodari wake na tunamtakia heri katika kipindi hiki.

Nd. Spika, mwenzetu mmoja ambaye alimsaidia sana Nd. Spika, katika Bunge lililopita, hayuko hapa pamoja nasi, kutokana na uamuzi wa wananchi. Naye ni Nd. John Kibogoyo. (*Makofi.*) Nd. Wabunge waliokuwamo katika Bunge la zamani natumaini mtakubaliana nami kwamba Nd. Kibogoyo aliifanya kazi ya kumsaidia Spika, kwa moyo safi na kwa bidii sana. (*Makofi.*) Namtakia heri Nd. Kibogoyo katika kazi ya kujenga taifa letu popote alipo. (*Makofi.*)

Nd. Spika, naomba tena kuchukua nafasi hii kuwapongeza wenzangu kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa Wabunge. (*Makofi.*) Nawapa pole wale ambao wamepitia msuko suko wa uchaguzi. Nd. Spika, hapa tupo wengine tuliokuwemo katika Bunge la zamani na wengine hii ndiyo mara yao ya kwanza kuwemo katika Bunge. Nd. Spika, nataka kuwahakikishia Nd. Wabunge wote kuwa sisi sote wapya. (*Makofi.*) maana hili ni Bunge jipya. Ni kweli baadhi yetu tumekuwa ndani ya Bunge la zamani tunaelewa vizuri zaidi taratibu za Bunge na katika hilo tutakuwa na msaada mkubwa kwa ndugu zetu. Lakini wenzetu nao wanalo la kutufundisha,

[Makamu wa Rais wa Chama cha TANU]

nalo ni mawazo mapya na namna ya kutekeleza vizuri siasa ya nchi yetu. Hilo ni kubwa zaidi. Sisi wenzetu tutakuwa wanafunzi tukikaa vizuri sana kuwasikiliza. Nd. Spika, kama tunavyojua Bunge ni shule kubwa sana ya siasa. Tunatumaini wote tutakuwa wanafunzi na pia tutakuwa waalimu. Yaani kwa kifupi tutashirikiana vizuri kwa faida ya Taifa letu. Ahsanteni sana. (*Makofi.*)

**Sheikh Thabit Kombo:** Nd. Spika, na Nd. Wabunge wenzangu wote. Mimi sitakuwa na mengi kwa sababu mambo yote kisha maliza Makamu wa Chama ambavyo kama alivyosema mwenyewe. Mimi nataka kusema kuwa leo tumepata bahati sisi Wabunge wapya sote kama alivyosema Ndugu hapa na dalili kwa wote ni wapya kwa vile sote tumeanza tena leo kula yamini. Ingekuwa tuko wa zamani—tungekuwa wa zamani tusije tena leo wakaja wapya. Lakini hivyo sote leo tunaanza tena mwanzo.

Sasa Nd. Spika, ilivyokuwa leo tumekula yamini ya mwanzo na tumetoa ahadi zetu hapa mbele ya Mwenyezi Mungu, ahadi hizi tumetoa kwa kutekeleza majukumu yetu tutakayopewa na Chama cha TANU na AFRO, pamoja na Serikali na sisi ni wajibu wetu kuyatekeleza kwa sababu tupo hapa katika Baraza hili kuwa sote pamoja, na sote ndugu pamoja na wajibu wetu sote kustahimiliana na kufundishana na kuelekezana yanayofaa. Kama alivyokwisha sema Ndugu hapa kuwa wale wa zamani tuliopata bahati bado tumo katika Bunge hili tangu na tangu na wenzetu waliokuja leo ni sisi tuliotangulia tangu na tangu tu tayari kuwasaidia wenzetu Kanuni za Bunge na mipango ya Bunge kama itakavyostahiki kuwafahamisha. Na sisi sote hapa tunategemea vile vile kufuata kanuni na uongozi wa Mwenyewe Spika, pamoja na kiongozi wetu wa Serikali anayeendesha Bunge hili, yeye mwenyewe Makamu wa Rais wa TANU. Na hatuna budi vile vile kumshukuru kwa uongozi wake bora wa miaka mingi kuliongoza Bunge hili. (*Makofi.*) Mumepita katika Bunge hili misukosuko mingi bila ya hiyo ya uchaguzi muliyopata katika vijiji, ingawa sisi wengine tumepata bahati ya kupita hivi hivi. Lakini wengi tunajua wamepata misukosuko ya uchaguzi. Maana yake uchaguzi ni kama vita. Uchaguzi ni vita. Katika vita hutoka bahati watu wanakwenda vitani wengine huko katika vita hurudi wakawa ma-Sajini, wakawa ma-Kapteni ili hali walikwenda kupigana, na risasi zimewakosa lakini hupata bahati wakarudi na vyeo. Na wengine bahati mbaya huenda ikawa wasirudi kabisa. Ndiyo mfano wa Bunge. Wengine wamekwenda katika uchaguzi wamerudi hapa leo tunao, na wengine rafiki zetu kama tulivyokwishasema—alivyokwishasema Makamu tumewakosa kama akina Mzee Kibogoyo na wengine hatunao. Lakini vile vile tunawatakia heri.

Sasa nikirudi tena Nd. Spika, nakupa pongezi wewe mwenyewe kwa jitihada yako kubwa ya kutuongoza katika Bunge hili kwa miaka yote uliyoanza, ingawa kwa muda kidogo ulipata mapumziko kwenda huko Dodoma. Sisi hatukusema kuwa ulikwenda kufanya kazi. Tunasema ulikwenda kupumzika. Leo umerudi tena hapa, sisi tutakuwa nawe kama ilivyokuwa tayari kushirikiana na tunatarajia uongozi wako na msaada wako na sisi tutakuwa tayari kukosolewa kwa sababu Bunge lina sheria yake na lina heshima yake. Huja mtu katika Bunge kifua wazisheria hii si sheria. (*Kicheko.*) Na tuna wenginewe, haidhuru leo ndiyo tunaanza kufundishana. Tunaona wengine wamekuja kula yamini hapa mashati yao vifua wazi. Tunaweza kusema maana yake jana tulisema kule katika T.P.P. kuwa Spika hatakuwa mkali. Tutasema naye awe mpole leo, lakini tunatumaini kwamba baada ya leo Wabunge wenzetu wale na hatuwalaumu maana yake ni wageni hawajui. Lakini sisi tulio wenyeji tusichelewe kumfundisha mwenzetu huko nje kuwa wewe babu unakwenda katika Bunge hivi si sheria itakuwa vibaya. Hivi ni matusi kwa Bunge. Lazima tuambizane huko nje kabla ya hapa maana yake—(*makofi*)—sisi wenyewe tutaona vibaya humu madhali ni Wabunge sote na sote ndugu kumwona mtu anainuliwa hapa anatolewa nje. Mimi wenyewe hapa zamani nilimwona siku moja Nd. Spika huyu huyu wala si mwingine akimtoa Nd. Bryceson hapa. Alivaa shati lake li wazi. Na yeye yupo mwenyewe. (*Kicheko.*) Akaambiwa si sheria akainuka hapa akatoka akaenda akavalia akaja. Nadhani sheria zile zingalipo. Sisi Wabunge wajibu wetu kuzifuata kwa sababu kama hatuzifuati itakuwa si makosa ya Spika. Tutakuwa tunakosea sisi wenyewe. Na natumai kwa ahadi tuliyotoa leo hapa Inshallah Mwenyezi Mungu atatusaidia, ataturahisishia kila yaliyo mazito juu yetu tuweze kutimiza majukumu yetu tuliyopewa na Serikali, kwa sababu tuna majukumu makubwa. Kila mtu ana jukumu lake. Wengine Mawaziri, wengine Wakuu wa Mikoa wengine Wenyeviti. Kila mmoja Mwenyezi Mungu atujalie yale majukumu tutakayopewa yawe rahisi juu yetu tuyaweze tupate kutimiza, wajibu wetu.

Mpaka hapa Nd. Spika, amshukuru kwa kunipa nafasi na mimi nikauagana na Nd. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutoa yanayofaa kuelezwa. Na sina shaka kwa niaba ya wenzangu watanikubalia tutakuwa sote tu tayari kutumikia kama tulivyoahidi katika hii yamini tuliyokula hapa maana yake yamini hii si nyepesi. Ni yamini kubwa. Yamini yenye ahadi. Siyo ile yamini ya kula tu Wallahi Ladhimu ukanyamaza. Wengine husema Wallah Ladhimu tu hapa. Husema Wallahi Laadhimu. Ile siyo. Hii tumetoa ahadi. Tumeapa kwa maneno ya ahadi kuwa tutatumikia, tutalinda, tutatetea na baadaye tena tumemtaja Mungu atusaidie. Kutusaidia maana yake atubariki kwa haya tuliyoyatamka na sina shaka kwa siku ya leo Mwenyezi Mungu atatubariki. Ahsante sana. (*Makofi.*)

**Nd. Julie Manning:** Nd. Spika, kwanza ningependa kutoa shukrani kwa kunipatia nafasi hii . . . .

**Nd. Spika:** Sogea kwenye chombo kingine. Hatukusikii vizuri.

**Nd. Julie Manning:** Nd. Spika, kwanza ningependa kutoa shukrani kwa kunipatia nafasi hii ya kusema machache kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge kwa miaka mitano ijayo. (*Makofi.*)

Naona hii ni heshima kubwa kwangu kwani kama unavyofahamu, Nd. Spika, pamoja na Wabunge wengine wenzangu, leo hii ni mara yangu ya kwanza kuingia Bungeni na leo hii nikatunukiwa nafasi hii fupi ya kutoa pongezi za kuchaguliwa kwako kuwa

Spika. Jambo hili linanipa moyo zaidi kwa sababu mwaka huu kama wote mnavyofahamu ni mwaka wa Wanawake. (*Kicheko.*) Na kwa kunipatia nafasi hii kusema machache katika kikao hiki cha kwanza kabisa inadhihirisha wazi kwamba Bunge hili nalo pia haliko nyuma katika jambo hili.

Nd. Spika, bila shaka Wabunge wenzangu watakubaliana nami kuwa hakuna mtu mwingine yeyote mwenye sifa zaidi kuliko zako kwa kustahili kuchaguliwa katika nafasi hii ya Spika. (*Makofi.*) Ninafahamu kuwa umewahi kuwa Spika wa Bunge hili tangu nchi yetu imepata uhuru na kwa hakika wewe ulikuwa ni mzalendo wa kwanza kushika cheo hiki cha u-Spika. (*Makofi.*) Umeendelea kuifanya shughuli hiyo mpaka mwaka 1973 ulipochaguliwa na Nd. Rais kuwa Waziri katika Wizara ya Ustawi shaji wa Makao Makuu Dodoma. Kwa ajili hii basi wewe si mgeni katika Bunge hili kama sisi wengine ila ni mwenyeji kabisa. Ninaamini kuwa ujuzi ulioupata kwa muda mrefu katika kuliongoza Bunge hili utatusaidia sisi sote.

Nd. Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza *Chief* Kasusura kuchaguliwa kuwa Naibu wa Spika. (*Makofi.*) Nimefahamishwa ingawa mimi sikuwako katika Bunge hili kuwa *Chief* Kasusura ni mara yake ya pili kuchaguliwa kuwa Naibu wa Spika.

Mwisho ningependa kuwapongeza Wabunge wote ambao wamechaguliwa kwa nija mbali mbali kuingia katika bunge hili. Nafikiri sitakosea nikisema kwa niaba ya Nd. Wabunge wenzangu kuwa tutashirikiana nawe wakati wote na katika kazi zote. Ahsante sana. (*Makofi.*)

**Nd. E. Sokoine:** Nd. Spika na Nd. Wabunge, mimi pia napenda kwanza nichukue nafasi hii ya kuungana mkono pamoja na wasemaji waliotangulia katika kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kwa mara ya tatu kuwa Spika wa Bunge la nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi.*)

Nd. Spika, uchaguzi tuliofanya leo hii asubuhi umedhihirisha wazi imani kubwa waliyonayo Nd. Wabunge wa zamani na wa sasa katika uongozi wako wa muda mrefu katika kuliongoza Bunge letu. Katika kipindi kilichopita, Nd. Spika, umekuwa Spika wa Mabunge mawili yaliyopita na sisi ambao tuliobahatika kuwa katika Bunge hili katika kipindi hicho chote tunakumbuka kazi njema na kazi ngumu uliyoifanya katika kuongoza majadiliano mbali mbali yaliyohusu maendeleo ya Taifa letu na katika kipindi hicho cha miaka kumi hatukumbuki hata siku moja, siku ambapo umeruhusu hasira au uchovu kukuongoza katika utekelezaji wa kazi zako. (*Makofi.*) Kila siku umetuongoza kwa busara katika kazi za kila siku na wakati tulipopotoka katika majadiliano mbali mbali hukusita katika kuturudisha katika mstari na wala hukuchoka hata siku moja kuanzia mazungumzo ya asubuhi mpaka usiku katika kutekeleza kazi uliyodhaminiwa kufanya na Nd. Wabunge. Na hii ndio sababu Wabunge wote isipokuwa labda mmoja wote wamekupigia kura zao kuonyesha ishara ya imani waliyonayo juu ya uongozi wako katika kuongoza majadiliano ya Bunge letu na hata huyo mmoja tunaamini kwamba kafanya hivyo kwa kupotoka tu na sio kwa kukusudia. Kwa sababu kwanza naamini kabisa kwamba mtu aliyempigia kura hakuwa katika mashindano ya kugombea kiti cha Spika na kwa hivyo ni wazi kwamba kura yake hiyo ameitoa huko kwa makosa. Na kwa hivyo, Nd. Spika, tunasema kwamba sisi ambao tumejua kazi yako kwa kipindi kilichopita cha miaka kumi tunatumaini kabisa kwamba katika kipindi kijacho cha miaka mingine mitano inayokuja tunachoomba, leo tunachoweza kusema ni kumwomba Mwenyezi Mungu akuongezee afya, akuongeze busara kusudi kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu mwenyewe uweze kuendelea kutuongoza katika kazi iliyo ngumu ya kulijenga na kuliimarisha Taifa letu katika kuliondoa katika hali ya umaskini na unyonge. (*Makofi.*)

Pia napenda nichukue nafasi hii katika kumpongeza *Chief* Kasusura ambaye kwa muda mrefu katika kipindi kilichopita pia alikuwa ni Naibu wako. Naye unaamini kabisa kwamba amekwishaonyesha uwezo wake katika kazi za kuongoza shughuli za kazi za Bunge na nasema tunaloweza kusema sisi Wabunge ni kwamba tunawaahidi ninyi wote wawili kwamba tutawapa moyo wa ushirikiano ili kutoifanya kazi yenu iwe ngamu. (*Makofi.*)

Jambo la mwisho kabisa ambalo ningependa niseme ni kwamba kwa Nd. Wabunge wenzangu ambao tumeingia katika Bunge hili kwa njia mbali mbali tunajua kwamba sisi tumechaguliwa miongoni mwa watu wengi. Tumechaguliwa miongoni mwa maelfu ya Watanzania wengine wakulima na wafanyakazi ambao tumewaacha huko vijijini. Hii haina maana kusema kwamba sisi ni bora sana kuliko wengine. Maana yake peke yake kuchaguliwa kwetu kuja hapa ni kwamba kutokana na tabia za binadamu haiwezekani kwa watu wote kuwa viongozi. Ni lazima watu wachache miongoni mwa wengi wachaguliwe wapewe madaraka waaminiwe na wafanye kazi kwa niaba ya wengine. Na ndio sababu sisi tuko hapa. Na sisi hatuna cho chote wala njia ye yote ya kuweza kulipa shukrani zetu kwa wananchi Watanzania wakulima na wafanyakazi ambao wametuamini na wametuleta hapa katika Bunge. (*Makofi.*) Njia ya pekee ambayo tunaweza tuhakikisha kwamba tunalipa shukrani hiyo ni kwamba kile tulichokiomba tunafanya na kutekeleza kwa moyo wa kweli. (*Makofi.*) Kwa sababu tuligombea kuchaguliwa kuwa Wabunge, lakini kuwa Mbunge peke yake hakuna maana. Maana hatukugombea kuja hapa kusudi tupate sifa. Tulichogombea ni kupata nafasi ya kutumikia watu wetu na hiyo ndiyo shukrani pekee ambayo tunaweza tukawaonyesha wakulima na wafanyakazi wa-tanzania. Na kwamba katika miaka mitano inayokuja ambapo tutakuwa hapa katika Bunge hatukuja hapa kwa sababu ya kushindana kusema au kuonyesha uhodari wa kusema, kutafuta sifa na kadhalika, lakini tumekuja kwa sababu ya kutafuta kuwatumikia wananchi. Sasa katika kipindi hicho cha miaka mitano tunaweza tukawa tumestahili sifa hiyo ya wananchi, imani hiyo waliyotupa iwapo katika matendo yetu, iwapo katika yote tutakayozungumza katika Bunge hili yatakuwa na maana ya kusaidia kuinua hali ya maisha ya wakulima na wafanyakazi wa Tanzania. Iwapo katika matendo yetu, iwapo katika kusema kwetu, hayo tutakayoyasema, tutakayoyatenda, kama hayatakuwa na shabaha na lengo ya kufanya maisha ya Watanzania yawe bora zaidi kuliko yalivyo sasa, basi U-bunge wetu utakuwa hauna thamani yeyote. Kwa hivyo, nasema kwamba, sisi mbali na

[Nd. E. Sokoine]
kujipongeza kwamba tumepata ushindi baada ya kupita misukosuko mikubwa lakini nafikiri kitu kikubwa ni kukumbuka kwamba tunaweza tukawaonyesha wananchi wa Tanzania wakulima na wafanyakazi waliotuleta hapa tunaweza tukawalipa kwa njia mbili tu. Kwanza ni hiyo ya kuwapa kuwatumikia kwa moyo wote. Moyo usio na uchoyo katika kipindi chote hiki cha miaka mitano tutakapokuwa viongozi wao. Na pili katika kukumbuka kwetu kwamba sisi ni viongozi wa Vyama vyetu vya TANU na *AFRO-SHIRAZI* na kwamba daima katika uongozi wetu tutazingatia siasa ya Vyama vyetu vya TANU na *AFRO-SHIRAZI* katika kuwatumikia wananchi wa Tanzania. Na kama tukikumbuka haya tunaweza tukatekeleza mkataba wetu vizuri na wananchi katika kipindi hiki kinachokuja cha miaka mitano. Ahsante Nd. Spika. (*Makofi.*)

**Spika:** Nd. Wabunge, kabla ya kuliahirisha Bunge, ningependa kuwakumbusha kwamba kanuni za Bunge haziruhusu kuvaa *uniform* katika Bunge. Lakini natambua kwamba wale Ndugu waliovaa walivaa kwa nia njema na kutokufahamu kanuni za Bunge. Kwa hiyo nawakumbusha kwamba tutakapokutana saa mbili usiku leo, wavae nguo za kawaida ambazo zinaruhusiwa na Bunge. (*Makofi.*)

Kwa hiyo, Nd. Wabunge, naliahirisha Bunge hili paka saa mbili za usiku.

(*Bunge lilifungwa saa 7.30 mchana mpaka saa 2.00 usiku*).

(*Saa mbili ya usiku Bunge lilirudia*)

## UCHAGUZI WA WABUNGE WA TAIFA WA MIKOA

Mkoa wa Dar es Salaam.
Mkoa wa Dodoma.
Mkoa wa Iringa.
Mkoa wa Kigoma.
Mkoa wa Kilimanjaro.
Mkoa wa Lindi.
Mkoa wa Mara.
Mkoa wa Mbeya.
Mkoa wa Morogoro.
Mkoa wa Mtwara.

## KUAHIRISHA BUNGE

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika naomba Bunge liahirishwe mpaka kesho saa kumi jioni.

**Nd. A. Tandau:** Nd. Spika naafiki.

(*Saa tatu na nusu usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 7 Novemba, 1975 saa kumi jioni*).